



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NZEGA



Unapo jibu Tafadhali taja:
Kumb. Na.NTC/A4/11/78

17/09/2021,

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI.

Rejea mada tajwa hapo juu.

2. Kufuatia Tangazo la Ajira lenye **Kumb Na. NTC/CA4/2/80** la tarehe **24/08/2021** lililohusu nafasi ya **Mtendaji wa Mtaa Daraja la III** na **Dereva Daraja la II**, Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Nzega inawatangazia Waombaji wote wa nafasi ya Mtendaji wa Mtaa Daraja la III na Dereva Daraja la II waliokidhi sifa na vigezo kufika kwenye usaili.
3. Usaili wa **Mtendaji wa Mtaa Daraja la III** utafanyika tarehe **27/09/2021** Saa mbili kamili (02:00 Asubuhi) katika Ukumbi wa Halmashauri uliopo Kata ya Kitangili, Kijiji cha Budushi, Kitongoji cha Ipazi Wilayani Nzega.
4. Usaili wa **Dereva Daraja la II** utafanyika tarehe **28/09/2021** Saa mbili kamili (02:00Asubuhi) katika Ukumbi wa Halmashauri uliopo Kata ya Kitangili, Kijiji cha Budushi, Kitongoji cha Ipazi Wilayani Nzega.
5. Waombaji wote wanatakiwa kufika na Vyeti halisi (Original Certificates) vya Mafunzo, Ujuzi na Cheti cha kuzaliwa. Aidha Muombaji atakayekuja na "Transcript", "Result Slip" pekee bila vyeti halisi hataruhusiwa kufanya Usaili.
6. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe wanakuja na Uthibitisho kutoka **TCU** na **NACTE**.
7. Waombaji wote ambao hawajaona majina yao hawakukidhi vigezo hivyo wanashauriwa kuomba tena nafasi zitakapo tangazwa.
8. Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Nzega haitahusika na gharama zozote za waombaji katika kipindi chote cha Usaili (Usafiri, Chakula na Malazi).
9. Orodha ya Majina ya Wasailiwa imeambatanishwa

Shomary S. Mndolwa,
MKURUGENZI WA MJI
NZEGA.

MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
NZEGA.

